TUANZE

1. Maswali ya kujibu:

a. Kwa nini unapenda kufunzwa?

b. Unawaza inaamanisha nini kuwa mfwasi wa Yesu?

c. Unatarajia kufaidia nini kutokana na mafundisho haya?

2. Amri kuu ya Mungu:

Amri kuu inapaswa kuwa ya muhimu katika vyote tunavyosema au kufanya.Wakati Yesu aliulizwa amri gani ilikuwa kuu, alijibu: “Akamwambiya, mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako na kwa akili zako zote.Hii ndio amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza.Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, mpende jirani yako kama nafsi yako.Katika amri hizi mbili hutegemea torati yote na manabi.”

(Mathayo 22:37-40, BTK)

3. Kazi kuu ya Mungu:

Amri kuu ni ya maana sana katika kutimiza kazi kuu.Kazi hii kuu inalenga wote walioamini Kristo, kwani Yesu alisema: “Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho mtakatifu; na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote hata ukamilifu wa dahari.”

(Mathayo 28:19-20, BTK)

4. Maana ya Mfuasi/Mwanafunzi:

Neno ya kigiriki inayomaanisha mwanafunzi, *mathes*, haimaanishi tu “kujifunza”.Lakini ni kuungana na mwalimu wako na kuwa mfuasi wake katika yale anayoyaamini na katika tabia.

Mtume Paulo alisema, “Mnifuate mimi kama ninavyomfuata Kristo.

5. Maana ya Mkufunzi au Mwalimu (Mfanya Wafuasi):

Huyu ni mtu aliyefunzwa na kuhitimu na kuwa na silaha zote ili kuwafundisha wengine katika hali sawa na yake.

(Wakoritho 1 11:1, BTK)

Bwana Yesu alisema, “Mwanafunzi hawi mkuu kuliko mwalimu wake, lakini kila mtu ambaye amehitimu hulingana na mwalimu wake.”

(Luka 6:40, BTK)

6. Maana ya Kufanya Wafuasi:

Kufanya wafuasi ni hatua ya kujiweka wa kujiingizia (kwa mfano tabia, mwendo wa hali zako) katika watu wengine ukitarajia mavuno kutokana na kujitoa kwako.

(Luke 6:40, BTK)

UTAMBULIZI

1. Kusudi :

a. Kuwa mwanafunzi wa Kristo Yesu aliyekomaa kwa kutenda Nidhamu tano (5) za Kiroho
b. Kuwa mwenye nidhamu mwaminifu waYesu kwa kuzalisha zile Hatua 8

2. Sehemu:

a. Hatua 1-3 - *Ombi*
b. Hatua 4-8-*Safari*

3. Kazi ya akili:

Ombi ya Kujitoa na maandiko yanayousiana na *Safari*

4. Masomo ya ziada:

Ombi ya Kujitoa na habari zinazousiana na *Safari*

5. Vifaa vya Mafundisho ya Biblia:

Utimisho wa vifaa katika Mafundisho ya Biblia na vile vile kwa yale yanaopatikana katika mtandao

6. Vifaa vya Kusoma:

a. Injili ya Yohana iliyoandikwa na Mtume Yohane
b. Barua kwa Warumi iliyoandikwa na Mtume Paulo
c. The Master Plan of Evangelism(Mpango Mkuu wa Uinjilisti)iliyoandikwa na Robert Coleman

7. Kazi ya ziada - Hatua 1:

a.*Nidhamu 1: Mwabudu Bwana:* Mwinue/Msujudu-Mwongozo wa Maombi 1-6
b.*Nidhamu 2: Sikiliza Neno Lake:* Soma/Tafakari -Yohana 1-7 (mlango moja kwa siku)
c.*Nidhamu 3: Omba Mapenzi Yake*: Tambua/Itikia -Yohana 1-7 (mlango moja kwa siku)
d.*Nidhamu 4: Ungana na Watu Wake:* Mfanya wafuasi, Washiriki wenzako, na Mufuasi anayewezekana
e. *Nidhamu 5: Elezea Dunia:* Changia ushuhuda wako na angalau mtu 1
f. The Master Plan of Evangelism : Mlango wa 1 – Soma/Tia alama
g. Ombi ya Kujitoa: Sehemu ya 1: Tia akili/Tafsiri/Tia katika matendo
h. Mafundisho ya Biblia ya Kibinafsi: Angalia mapendekezo; kisha chagua moja

OMBI YA KUJITOA

Mungu, nimetambua kwamba nimetenda dhambi, na kwamba dhambi zangu zimenitenga Nawe. Nakuja kwako na toba na napokea msamaha wako kupitia Kristo.

Yesu naamini ulikufa msalabani kwa ajili yangu na naugana nawe katika kufa kwa dhambi. Naamini ulifufuka kutoka kaburi kwa ajili yangu na naungana nawe katika ufufuko kwa uzima wa milele, ambao uliupana kwa neema kupitia imani.

Nakuchukua wewe, Yesu, kama Bwana na Mwokozi, kuwa nawe na kukusika kwanzia leo na siku zote; kwa mema, na kwa mabaya; kwa utajiri, wala umasikini; katika magonjwa na katika afya; Kukataa wengine na kushikamana na wewe tu mpaka umilele yote;

Nakupatia maisha yangu, na napokea Roho Wako.

MWONGOZO WA MAOMBI Simameni, jueni kwamba mimi ndimi Mungu… (Zaburi46:11)

1. Umilele – Uwepo wako ni wa milele na milele
Tangu milele, hata milele ndiwe Mungu. (Zaburi 90:2) **2. Muumbaji – Uliumba vyote bila chochote**
Hapo mwanzo, Mungu aliumba mbingu na dunia. (Mwanzo 1:1) **3. Mtawala Mkuu – Unatawala juu ya uumbaji wote** Yeye aliyehimidiwa, mwenye uweza peke yake, Mfalme wa wafalme, Bwana wa mabwana. (Timoteo 1. 6:15)

4. Bwana – Unaongoza uumbaji wote
Bwana ameweka kiti chake cha enzi mbiguni, na ufalme wake unavitawala vitu vyote. (Zaburi 103:19)

5. Mtakatifu – Wewe ni mkamilifu
Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ni Bwana wa majeshi, dunia yote imejaa utukufu wake. (Isaya 6:3)

6. Mungu – Ni wewe pekee
Mimi ni mwanzo, na mimi ni wa mwisho; zaidi yangu mimi hapana Mungu. (Isaya 44:6)

7. Mwenye nguvu – Unafanya chochote wakati wowote
Kisicho wezekana kwa mwanadamu kwa Mungu kinawezekana. (Luka 18:27)

8. Nipo popote-Upo pahali pote kwa wakati mmoja
Kama ningepanda mbinguni, wewe uko; ningefanya kitanda kuzimu, wewe uko. (Zaburi 139:8)

9. Anayejuwa vyote-Unaelewa vitu vyote na watu wote
Jinsi zilivyo kuu utajiri na hekima na maarifa ya Mungu, hukumu zake hazichunguziki, wala njia zake hazitafutikani. (Warumi 11:33)

10. Mwenye upendo - **Unajali bila kuangalia hali na bila mwisho**
Kwa maana ginsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtowa Mwana wake wa pekee.(Yohana3:16)

11. Natambua Ukuu Wako
Bwana ndiye Mkuu Mwenye kusifiwa sana, wala ukuu wake hautambulikani. (Zaburi 145:3)

12. Nashukuru/Nafurahia wema wako
Mshukuruni Bwana kwa kuwa ni mwema; kwa maana fadhili zake ni za milele. (Zabuzi 136:1)

13. Baba wa milele yote – Unalinda na kusughulikia/Kuhangaikia
Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, msaada utakao onekana tele wakati wa mateso (Zaburi 46:1)
Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu. (Wafilipi4:19)

14. Ndugu wa umilele yote – Unakomboa na kurejesha
Katika yeye huyo, kwa damu yake; tunao ukombozi wetu, msamaha ya dhambi, sawa sawa na wingi wa neema yake. (Waefeso 1:7)
Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama!Yamekuwa mapya. (Wakorinto 2, 5:17)

15. Mpenzi wa umilele yote - Unafariji na kuukumu
Nami nitamwomba Baba naye atawapa msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele. (Yohana 14:16)
Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu. (Yohana 16:8)

16. Nioshe /Nitakase
Unioshe kabisa na uovu wangu, unitakase dhambi zangu. (Zaburi 51:2)

17. Nijaze
Mkajazwe na Roho. (Waefeso 5:18)

18. Niongoze
Neno lako ni taa miguuni pangu na mwangaza kwa njia zangu. (Zaburi 119:105), (Yote BTK)

NIDHAMU 5 ZA KIROHO



Za juu 5	**Nidhamu za Kiroho**	**Misahiri ya Msingi**
Nidhamu# 1	**Mwabudu Bwana**	**Yohana 4 :24**
« Mungu ni roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli. »		
Nidhamu # 2	**Sikiliza Neno Lake**	**Yohana 8 :31**
« Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli. »		
Nidhamu # 3	**Omba Mapenzi Yake**	**Yohana14 :13**
« Nanyi mkiomba lolote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. »		
Nidhamu # 4	**Ungana na Watu Wake**	**Yohana15 :12**
« Amri yangu ndio hii, mpendane, kama nilivyowapenda ninyi. »		
Discipline # 5	**Elezea Dunia**	**Jean 20 :21**
« Amani iwe kwenu; kama Baba alivyonituma mimi, mimi nami nawapeleka ninyi. »		

❖ Maandiko yaliyo nukuliwa yametoka katika tafsiri ya Biblia Takatifu (BTK)

SAFARI

Safari ni kifaa au chombo cha uinjilisti ambayo itakusaidia kushuhudia imani yako na wengine kwa urahisi. Inaonyesha ginsi gani Kristo alilipa dharama ya dhambi na kuurejesha au kurekebisha uhuusiano wetu na Mungu ambao ulikuwa umevunjika. Kuna sehemu tano ya *Safari*, na kila mmoja inasindikizwa na andiko na mfano wakuufanana. Maneno yafuatayo yanaeleza maana ya *Safari*:

1) *Tatizo* katika maisha ni dhambi, wote wanahukumiwa dhambi.
2) *Hukumu* ambayo inatokana na hii shinda ni kifo.
3) *Gharama/Malipo* ya dhambi inatokana na kifo cha Yesu.
4) *Njia/Hatua* ya kupokea malipo haya ni imani.
5) *Kusudi/Lengo* ambayo inafuata imani ni upendo kwa Mungu na watu.

Mistari yenyi ku support *Safari* yametoka katika barua ya Paulo kwa Warumi.
Mfano huu wa mchoro inarahisisha kuonyesha unapoongea na wengine watu kuuhusu *Safari.*



Maneno	Andiko la kutia akilini	Mifano
***Tatizo* ni DHAMBI**	**Warumi 3 :23**	**Darts/Dartsboard**
« Kwa maana wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu na Mungu. »		
***Hukumu* ni KIFO**	**Warumi6 :23**	**Mshahara/Talanta**
« Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo yesu Bwana wetu.»		
***Malipo* ni KRISTO**	**Warumi 8 :3**	**Hukumu/Haki**
« Maana yale yasio wezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, Mungu kwa kumtuma mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi katika mwili, alihukumu dhambi katika mwili.»		
***Hatua/Njia* ni IMANI**	**Warumi 10 :9**	**Check/Cash**
« Ukikiri katika kinywa chako kwamba yesu ni bwana, na kuamini katika moyo wako yakwamba Mungu alimfufua katika wafu, utaokolewa. »		
***Kusudi/Lengo* ni UPENDO**	**Warumi 13 :10**	**Tia hazina/Rudisha**
« Pendo halimfanyi jirani neno baya; basi pendo ndio utimilifu wa sheria.»		

- Maandiko yaliyo nukuliwa yametoka katika Tafsiri ya Biblia Takatifu (BTK)

MIFANO KATIKA SAFARI

1. <u>Darts/Dartboard</u> inaonyesha *Shida/Tatizo*, ambayo ni DHAMBI: Mungu ni Upendo na Kutokana na upendo alikuumba ukapate kufurahia uhusiano wakibinafsi pamoja naye milele, lakini upendo wa kweli inapashwa kuwa huru kuchaguwa katika ya faida za Mungu au za mtu binafsi. Kwa huzuni na kwa bahati mbaya tulichagua kujifurahisha kabla yakumfurahisha Mungu, na pale tukaleta shinda na utengano kati yetu na Mungu. Tazama mchezo wa mkuki ambao mtu anatakika kuudona katikati ya kibao kila mara ili kushinda.Ukidona katikati mara nne juu ya mara tano na mimi nikidona mara moja, nani ni mshindi ?Hakuna kati yetu aliyeshinda, kwa sababu sheria ni kwamba kudona katikati mara tano. Kiwango cha Mungu ni ukamilifu; kwa hivyo, dhambi moja inatosa kututenga na Mungu.

2. <u>Mshahara/Zawadi</u> inaonyesha *Hukumu/ Ghadhabu*, ambayo ni KIFO:

Kama unakibarua unapata malipo kwa kazi unayoifanya, na kinyume ya yale zawadi sio kitu ulichokistahili wala mshahara, lakini unaipokea tu kutokana na kupenda kwa mtu mwengine.Tumepokea mshahara sawa kifo kwa kazi zetu za dhambi kwa Mungu, lakini amechagua kutupatia zawadi ya uzima kwa gharama ya mwana wake, Yesu Kristo.

3. <u>Hukumu/Haki</u> inaonyesha *Malipo*, ambayo ni KRISTO:

Unafungwa kwa kosa ambalo hukumu yayo ni kifo. Unapofika kotini, hakimu anakuuliza kama uko mwenye kosa au hapana. Ukijuwa kama ushahindi ulio ni mwingi unajibu, «Nakubali makosa yangu mhesimiwa. » Na hakimu anakuhukumu na hukumu yako ni kifo.Na unajihisi hauna tumaini, mpaka pale unasikia sauti ya hakimu akisema, « Kungali na tumaini kwa ajili yako. » Hakimu anasimama na anajogea pembeni yako na anasema «Nitalipa gharama kwa ajili yako na maisha yangu ili yakwamba upate haki, na ukapate kuwekwa huru. » Mungu ni hakimu aliyekuja dunia katika mwili kama Yesu kwa kulipa gharama kwa ajili ya dhambi zetu kwa kukufa msalabani kwa ajili yetu.

4. <u>Check/Cash</u> inaonyesha *Hatua* ambayo ni IMANI:

Uliitika malipo kutoka kwa mtu kupitia njia ya check, pale unaonyesha imani kwa yule mtu na unaamini kwamba anakiwango cha pesa za kutosha kwenye account yake ili apate kukulipa.Na hata vile ile check haina faida hadi pale hutakapo chukua hatua na kwenda kwenye benki na kuigeuza ile check iwe cash. Na vile vile imani katika Mungu sio kujuwa tu zawadi yake ya uokovu, lakini ni kuitumika kwa kuamini Kristo ili akupatie kwa kweli kile ambacho hupana ambao ni uzima wa milele.

5. <u>Wekesha/Rudisha</u> inaonyesha *Lengo/Kusudi* ambayo ni UPENDO:

Unapowekesha pesa kwenye kampuni, unafanya hivyo kwa matarajia kwamba zitarudia. Na hii ndio lengo la kila anaye wekeza.Wakati Mungu anawekeza upendo wake ndani yako kupitia katika kafara ya Mwana wake na nguvu za Roho wake, na anatarajia tukapate kumrudishia. Anachotarajiya kwetu ni upendo. Lengo la Mungu ni kuzalisha upendo wake ndani yetu. Na jukumu letu katika maisha ni kumuruhusu.

Safari ya kwenda mbali na Mungu inatokana na dhambi zako.

Safari kuelekea kwa Mungu ni kupitia imani kwa Kristo Yesu.

HATUA YA 1

1. Soma *Ombi ya Kujitoa* mara Kadhaa kila siku.
2. Tia akilini Sehemu ya 1 ya *Ombi ya Kujitoa*.
3. Taja Maneno Msingi katika Sehemu ya 1 kwa kuchagua yalio bora katika kamusi (dictionary).

Mungu, natambua yakwamba mimi ni mtenda dhambi, na kwamba dhambi zangu zimenitenga na wewe.

Nakuja kwako na toba na napokea msamaha wako kupitia Kristo.

Maneno Msingi	**Maana / Tafsiri**
Kutambua	
Dhambi	
Kutenga	
Toba	
Kupokea	
Msamaha	
Krsito	

4. Tafsiri Sehemu ya 1 ya *Ombi* kwa akili zako mwenyewe.

5. Tia katika matendo Sehemu ya 1 ya *Ombi* katika maisha yako.

6. Kazi ya ziada – Hatua 2:

a. *Nidhamu 1: Mwabudu Bwana:* Muinue/Msujudu-Mwongozo wa Maombi 1-12
b. *Nidhamu 2: Sikiliza Neno Lake:* Soma/Tafakari - Yohana 8-14 (mlango moja kwa siku)
c. *Nidhamu 3: Omba Mapenzi Yake:* Tambua/Itikia - Yohana 8-14 (mlango moja kwa siku)
d. *Nidhamu 4: Ungana na Watu Wake:* Mfanya wafuasi, Washiriki wenzako, na Mufuasi anayewezekana
e. *Nidhamu 5: Elezea Dunia:* Changia ushuhuda wako na angalau watu 2
f. The Master Plan of Evangelism : Mlango wa 2 – Soma/Tia alama
g. Ombi ya Kujitoa: Sehemu ya 2 -Tia akilini/Tafsiri/Tia katika Matendo
h. Jifunze Biblia- Uwe na uzoefu na Yote yaliomo.

HATUA YA 2

1. Soma *Ombi ya Kujitoa mara* kadhaa kila siku.
2. Tia akilini Sehemu ya 2 ya *Ombi ya Kujitoa.*
3. Taja Maneno Msingi katika Sehemu ya 2 kwa kuchagua yalio bora kutoka katika kamusi (dictionary).

Yesu, naamini ulikufa msalabani kwa ajili yangu, na naungana nawe katika kufa kwa dhambi maishani mwangu.Naamini ulifufuka toka kaburini kwa ajili yangu na naungana nawe katika ufufuko kwenye uzima wamilele, ambao uliupana kwa neema kupitia imani.

Maneno Msingi	**Maana / Tafsiri**
Amini	
Ungana	
Kifo	
Ufufuko	
Uzima wa milele	
Maisha	
Neema	
Imani	

4. Tafsiri Sehemu ya 2 ya *Ombi ya Kujitoa* kwa maneno yako.

5. Tia katika matendo Sehemu ya 2 ya *Ombi ya Kujitoa* katika maisha yako.

6. Kazi ya ziada – Hatua 3:

a. *Nidhamu 1: Mwabudu Bwana:* Mweshimu/Msujudu-Mwongozo wa Maombi 1-18
b. *Nidhamu 2: Sikiliza Neno Lake:* Soma/Tafakari - Yohana 15-21 (mlango moja kwa siku)
c. *Nidhamu 3 : Omba Mapenzi Yake* : Tambua/Itikia - Yohana 15-21 (mlango moja kwa siku)
d. *Nidhamu 4: Ungana na Watu Wake:* Mkufunzi, Washiriki wenzako, na Mufuasi anayestahili.
e. *Nidhamu 5: Elezea Dunia*: Changia ushuhuda wako na angalau watu 3
f. The Master Plan of Evangelism: Mlango wa 3 – Soma/Tia alama
g. Ombi ya kujitoa: Sehemu ya 3 - Soma/Tafsiri/Tia katika matendo
h. Jifunze Biblia- Uwe na uzoefu na Uiingilia vya Vitabu

HATUA YA 3

1. Soma O*mbi ya Kujitoa* mara kadhaa kila siku.
2. Tia akilini Sehemu ya 3 ya *Ombi ya kujitoa.*
3. Taja Maneno Msingi katika Sehemu ya 3 kwa kuchagua yalio bora kutoka katika Kamusi (dictionary).

Nakuchukuwa wewe, Yesu, kama Mwokozi na Bwana, kukuwa nawe na kukushika kuanzia leo na siku zote; kwa mema, na kwa mabaya; kwa utajiri, na kwa umasikini ; katika magonjwa na katika afya; nikikataa mengine yote nikishikana nawe katika umilele yote;
Nakupatia maisha yangu, na napokea Roho wako.

Maneno Msingi	**Maana**
Mwokozi	
Bwana	
Kukushika/kushikamana	
Kukataa/kuacha	
Umilele	
Kupatia	
Maisha	
Roho	

4. Tafsiri Sehemu ya 3 ya *Ombi* kwa kwa maneno yako.

5. Tia katika matendo Sehemu ya 3 ya *Ombi* katika maisha yako.

6. Kazi ya ziada – Hatua 4:

a. *Nidhamu 1: Mwabudu Bwana:* Tazama kwa kina Ukuu wa Mungu na Uzuri wake
b. *Nidhamu 2: Sikiliza Neno Lake:* Soma Warumi 1-3/Tia akilini Warumi 3:23
c. *Nidhamu 3 : Omba Mapenzi Yake* : Mwitikie Mungu unaposoma Warumi 3:21-23
d. *Nidhamu 4: Ungana na Watu Wake:* Jiingize katika Ushirika na Ufuasi
e. *Nidhamu 5: Elezea Dunia:* Changia ushuhuda wako na angalau watu 3
f. The Master Plan of Evangelism : Mlango wa 4 – Soma/Tia alama
g. Jifunze Biblia- Uwe na uzoefu na Concordance

HATUA YA 4

Tatizo

Mungu | ***Sisi***

Upendo **<u>Dhambi</u>**

1. Rudilia *Ombi ya Kujitoa* na Warumi 3:23
2. Soma *Safari* katika ukurasa wa 4 na *Mifano ya Safari* katika ukurasa wa 5
3. Jufunze Mfano 1 – *Darts/ Dartboard*
4. Omba ufunuliwe unapotazama, Tafsiri na Kuitia katika Matendo Warumi 3 :21-23
5. Mtazamo – Warumi 3:21-23
Soma ukurasa katika tafsiri mbili na uone katika *mtazamo mkubwa*.
Andika mtazamo wako uambatane na *mtazamo mkubwa*. Hakikisha ni mtazamo ambao umetoka kwako binafsi bila kuuga au kufasilia kitabu.

6. Utafsiri – Warumi 3:21-23
Tafsiri kila mstari ukitumia mawazo yako na vifaa vyako vya mafunzo ya Biblia. Chagua maneno Msingi fulani, na utafute maana yayo katika kamusi (dictionary).

3:21 Lakini sasa, haki ya Mungu imedhihirika pasipo sheria; inashuhudiwa na Torati na Manabii; – (BTK)

Maneno Msingi & Maana:

Utafsiri:

3:22 Ni haki ya Mungu iliyo kwa njia ya imani katika Yesu Kristo kwa wote waaminio. Maana hakuna tofauti: (BTK)

Maneno Msingi & Maana:

Utafsiri:

3:23 : Kwa sababu wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu, (LSG)

Maneno Msingi & Maana:

Utafsiri:

7. Utumizi/Matumizi – Warumi: 3:21-23

Tumia/tumikisha ujumbe katika maisha yako ginsi Bwana atakuongoza. Hakikisha matumikio yako inaungwa mkono na maandiko na utafsiri wako.Chukua neno msingi uliyoiankika ili ikusaidie katika matumizi na uitie katika matendo katika juma mzima.

8. Kazi ya ziada-Hatua 5:

a. *Nidhamu 1: Mwabudu Bwana:* Tazama Ukuu wa Mungu na Uzuri wake
b.*Nidhamu 2: Sikiliza Neno Lake:* Soma Warumi 4-6/Tia akilini Warumi 6:23
c. *Nidhamu 3: Omba Mapenzi Yake:* Mwitikie Mungu unaposoma Warumi 4-6
d. *Nidhamu 4: Ungana na Watu Wake:* Jiingize/Jiusishe katika Ushirika na Ufuasi
e. *Nidhamu 5: Elezea Dunia*: Changia *Ombi* na angalau watu 3
f. The Master Plan of Evangelism: Mlango wa 5 – Soma na utie alama
g. Jifunze Biblia- Uwe na uzoefu na Vitu vilivyoshirikishwa(Cross References)

HATUA YA 5

Hukumu

Mungu ***Sisi***

Dhambi

Kifo

1. Rudilia *Ombi,* Mfano 1, Warumi 3:23, 6:23
2. Jifunze Mfano 2 -*Mshahara/Zawadi*
3. Omba ufunuliwe unapotazama, Tafsiri na Kutia katika Matendo Warumi 6 :21-23.
4. Mtazamo – Warumi 6:21-23
Soma ukurasa katika tafsiri mbili na uone katika *mtazamo mkubwa*.
Andika mtazamo wako uambatane na *mtazamo mkubwa.* Hakikisha ni mtazamo ambao umetoka kwako binafsi bila kuuga au kufasilia kitabu.

5. **Utafsiri – Warumi 6:21-23**
Tafsiri kila mstari kwa kutumia akili zako na vifaa vyako vya mafunzo ya Biblia. Chagua maneno msingi fulani, na utafute maana yayo katika Kamusi (dictionary).

6:21 Ni faida gani basi mliyopata siku zile kwa mambo haya mnayoyataharikia sasa? Kwa maana mwisho wa mambo haya ni mauti. (BTK)

Maneno Msingi & Maana:

Utafsiri:

6:22 Lakini sasa mkiisha kuwekwa huru, na kuwa mbali na dhambi, na kufanywa watumwa wa Mungu, mnayo faida yenu, ndiyo kutakaswa, na mwisho wake ni uzima wa milele. (BTK)

Maneno Msingi & Maana:

Utafsiri:

6:23: Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu, (BTK)

Maneno Msingi & Maana:

Utafsiri:

6. Matumizi – Warumi: 6:21-23

Tumia ule mshahiri katika maisha yako ginsi Bwana atakuongoza. Chagua neno msingi itakayo kusaidia kukumbuka matumizi na uitie katika matendo kwa juma mzima.

7. Kazi ya ziada-Hatua 6:

a. *Nidhamu 1: Mwabudu Bwana:* Tazama Ukuu wa Mungu na Uzuri wake
b. *Nidhamu 2: Sikiliza Neno Lake:* Soma Warumi 7-9/Tia akilini Warumi 8:3
c. *Nidhamu 3: Omba Mapenzi Yake:* Mwitikie Mungu unaposoma Warumi 7-9
d. *Nidhamu 4: Ungana na Watu Wake:* Jiusishe katika Ushirika na Ufuasi
e. *Nidhamu 5: Elezea Dunia:* Changia *Ombi* na angalau watu 3
f. The Master Plan of Evangelism : Mlango wa 6 – Soma na Utie alama
g. Jifunze Biblia- Uwe na uzoefu na Maandiko ya Biblia.

HATUA YA 6

Malipo

Yesu



1. **Rudilia** *Ombi,* Mfano 1-2, Warumi 3:23, 6:23, 8:3
2. **Jifunze** Mfano 3 - Hukumu/*Haki*
3. **Omba** ufunuo unapotazama, Tafsiri na Kutia katika Matendo Warumi 8:1-3.
4. **Mtazamo – Warumi 8:1-3**

5. **Utafsiri – Warumi 8:1–3**

   Tafsiri kila mstari ukitumia akili zako na vifaa vyako vya Mafundisho ya Biblia. Chagua maneno msingi kadhaa, na uchague maana bora zaidi kutokana Kamusi yako.

8:1 Sasa basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu. (BTK)

Maneno Msingi & Maana:

Utafsiri:

8:2 Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu umeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti. (BTK)

Maneno Msingi & Maana:

Utafsiri:

8 :3 Maana yale yasiyowezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwasababu ya mwili, Mungu, kwa kumtuma mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi, na kwa sababu ya dhambi aliihukumu dhambi katika mwili, (BTK)

Maneno Msingi & Maana:

Utafsiri:

6. Matumizi – Warumi: 8:1-3

Tumia ujumbe katika maisha yako ginsi Bwana atakuongoza. Chagua neno msingi itakayo kusaidia kukumbuka matumizi na uitie katika matendo juma mzima.

7. Kazi ya ziada-Hatua 7:

a. *Nidhamu 1: Mwabudu Bwana:* Tazama Ukuu wa Mungu na Uzuri wake
b. *Nidhamu 2: Sikiliza Neno Lake:* Soma Warumi 10-12/Tia akilini Warumi 10:9
c.*Nidhamu 3: Omba Mapenzi Yake:* Mwitikie Mungu unaposoma Warumi 10-12
d. *Nidhamu 4: Ungana na Watu Wake:* Jiunge katika Ushirika na Ufuasi
e. *Nidhamu 5: Elezea Dunia:* Changia *Ombi* na angalau watu 3
f. The Master Plan of Evangelism : Mlango wa 7 – Soma na Utie alama
g. Jifunze Biblia katika Mtandao: kuwa na mazoea na Greek Lexicon

HATUA YA 7

Hatua

Kristo



1. **Rudilia** *Ombi,* Mfano 1-3, Warumi 3:23, 6:23, 8:3, 10:9
2. **Jifunze** Mfano 4 - *Cash/Check*
3. **Omba** ufunuo unapotazama, Tafsiri na Kutia katika Matendo Warumi 10:8-10.
4. **Mtazamo – Warumi 10:8-10**

5. **Utafsiri – Warumi 10:8-10**
   Tafsiri kila mstari ukitumia akili zako na vifaa vyako vya Mafunzo ya Biblia. Chagua maneno ilio bora kutokana na Lexicon (ona mfano).

10:8 Lakini yanenaje, lile neno li karibu nawe, katika kinywa chako, na katika moyo wako; yaani ni lile neno la imani tulihubililo. (BTK)

Maneno Msingi & Maana:

neno 4487 *rhema*-kutoka katika *rheo*-kusema.Lile linalo semwa ao neno.

Utafsiri:

10:9 Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. (BTK)

Maneno Msingi & Maana:

Utafsiri:

10:10: Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata kaki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu, (BTK)

Maneno Msingi & Maana:

Utafsiri:

6. Matumizi – Warumi 10: 8-10

Tumia maandiko ku maisha yako ginsi Mungu anaongea na wewe. Chagua neno msingi itakayo kusaidia kukumbuka matumizi kisha huitie katika matendo kwa juma mzima.

7. Kazi ya ziada-Hatua 8:

a. *Nidhamu 1: Mwabudu Mungu:* Tazama Ukuu wa Mungu na Uzuri wake
b. *Nidhamu 2: Sikiliza Neno Lake:* Soma Warumi 13-16/Tia akilini Warumi 13:10
c.*Nidhamu 3: Omba Mapenzi Yake:* Mwitikie Mungu unaposoma Warumi 13-16
d. *Nidhamu 4: Ungana na Watu Wake:* Jiusishe na Ushirika na Ufuasi
e. *Nidhamu 5:* Elezea Dunia: Changia *Ombi* na angalau watu 3
f. The Master Plan of Evangelism : Mlango wa 8 – Soma na Utie alama
g. Jifunze Biblia- Jizoeshe/ Kuwa na uzoefu na vitu vyote vinavyo patikana

HATUA YA 8

Lengo

Yesu



1. **Rudilia** *Ombi,* Mfano 1-4, Warumi 3 :23, 6:23, 8 :3, 10:9, 13:10
2. **Jifunze** Mfano 5 - *Wekesha/Rudisha*
3. **Omba** ufunuo unapotazama, Tafsiri na Kutia katika Matendo Warumi 10 :8-10.
4. **Mtazamo – Warumi 13:8-10**

5. **Utafsiri – Warumi 13:8-10**

Tafsiri kila mstari ukitumia mawazo yako na vifaa vya Mafunzo ya Biblia. Chagua maneno ilio bora kutokana na Greek Lexicon.

13:8: Msiwiwe na mtu cho chote, isipokuwa kupendana, kwa maana ampendaye mwenzake ameitimiza sheria. (BTK)

Maneno Msingi & Maana:

Utafsiri:

13:9 Maana kule kusema, “usizini, usiue, usiibe, usitamani”; na ikiwapo amri nyingine yo yote, inajumlishwa katika neno hili, ya kwamba, mpende jirani yako kama nafsi yako. (BTK)

Maneno Msingi & Maana:

Utafsiri:

13:10: Pendo halimfanyii jirani neno baya; basi pendo ndilo utimilifu wa sheria (BTK)

Maneno Msingi & Maana:

Utafsiri :

6. Matumizi – Warumi: 13:8-10

Tumia ujumbe katika maisha yako ginsi Bwana anakunenea. Chagua neno msingi ili ikusaidie kukumbuka matumizi na kutia katika matendo katika juma mzima.

7. Kazi ya ziada kwa siku zijazo:

a.*Nidhamu 1: Mwabudu Bwana:* Endelea kumwabudu Mungu katika maombi yako ya kila siku

b. *Nidhamu 2: Sikiliza Neno Lake:* Endelea kusoma neno la Mungu na kulitafakari

c.*Nidhamu 3: Omba Mapenzi Yake:* Endelea kuomba Mapenzi Yake kama inavyo funuliwa katika Neno Lake

d.*Nidhamu 4: Ungana na Watu Wake:* Endelea kuungana na walio amini na kufanya wafuasi

e.*Nidhamu 5: Elezea Dunia:* Endelea kuongea kuhusu *Ombi* na *Safari*